

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 2 Mwaka wa 1

## 2 Kaini, Habili na Sethi

**Kwa Biblia** Mwanzo 4:1-16 na 25-26


### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba tufanye vile Mungu anataka sio tubadilishe na iwe vile tunataka.

### Somo

Baada ya Adamu na Hawa kufukuzwa kutoka kwa Bustani ya Edeni, hawakuenda kuishi mbali na hapo. Baadaye walipata mwana na Hawa alimuita Kaini. Labda Hawa alifikiri kwamba huyo ndiye mtu atakayezaliwa na awaokoe kutoka kwa adhabu ya dhambi yao. Adamu hakuelewa kwamba itakuwa mda mrefu ndio huyu mtu –Yesu –azaliwe. Mara tena akazaan mwana mwingine. Alimuiita Habili.

Kaini alikuua na akawa mkulima. Alikuza aina zote za matunda na mboga ya familia kukula. Habili alikuwa mfugaji, aliwapa familia yao nyama, ngozi na manyoya za mavazi.



### Maswali

1. Mwana wa Habili wa kwanza aliitwa nani?
2. Alipokua alifanya kazi gani?
3. Mwana wa Hawa wa pili aliitwa nani?
4. Alipokua alifanya kazi gani?
5. Mungu alitaka nini kama sadaka?
6. Kaini alitolea Mungu nini kama sadaka?
7. Habili alitoa nini?
8. Mbona Kaini aliua Habili?
9. Adhabu ya Kaini ilikuwa nini?
10. Mwana wa Hawa watatu aliitwa nani?

### Majibu

1. Kaini
2. Mkulima
3. Habili
4. Mfugaji
5. Mwana kondoo
6. Mboga
7. Mwana kondoo
8. Alikasirika kwa sababu Mungu alifurahia sadaka ya Habili wala si yake
9. Hatakuza chochote. Kila mtu atamchukia
10. Sethi



Katika somo lililopita, tulijifunza kwamba Adamu na Hawa walikuwa wachinje mwana kondoo wakati wamefanya kosa lolote. Labda kulikuwa na madhabahu karibu na makerubi iliyokuwa na upanga wa moto kando ya Bustani ya Edeni.

Madhabahu ni meza ilijoengwa kwa mawe makubwa. Mwana kondoo alichinjwa na kuchomwa kwa moto kwenye madhabahu. Wakati mwingine kama wamefurahi walikuwa wakimtolea Mungu mwana kondoo wa shukrani na kuonyesha upendo wao kwake.

Siku moja Kaini na Habili walitaka kumtolea Mungu sadaka. Habili alitii Mungu. Alichukuwa mwana kondoo kutoka kwa kundi lake na akatolea Mungu. Kaini hakukuwa na mwana kondoo kwa sababu alikuwa mkulima. Hakujali maneno yenye Mungu alikuwa amewaagiza. Badala yake lichukuwa baadhi ya mboga.

Kaini aliweka mboga zake juu ya madhabahu. Alingoja Habili naye alete mwana kondoo wake. Mungu alifurahia sadaka ya Habili lakini hakukubali ya Kaini. Mungu alikuwa amesema lazima kuwe na damu ya mwana kondoo. Mboga haikukuwa nzuri. Mungu akitaka kitu, si vizuri kubadilisha na kufanya tofauti. Lazima tufuate maagizo ya Mungu na tufanye vile amesema.

Kaini alikasirika. Alikasirika zaidi sana alipojua amekosa. Alipoona Habili amemwongoja, alikasirika na akamshabulia. Alimpiga mpaka akaanguka chini. Aliendelea kumpiga na akamua. Kaini alipoona Habili amelala kimya, aliogopa. Hakukuwa na mtu aliyekufa hapo awali. Kaini alikuwa na mshtuko mkuu alipoona Habili amekufa. Alizika Habili mafichoni na akaenda nyumbani.

Adamu na Hawa walikuwa wamejaribu kujifija kutoka kwa Mungu. Lakini hauwezi kujificha kutoka kwa Mungu. Mungu alimuona Kaini akiua Habili. Kaini alisikia sauti ikimwita, "Kaini! Kaini! Wapi nduguyo Habili?" Kaini aliogopa sana na akajibu, "Sijui, Habili ni mtu mzima anatakiwa ajilinde mwenyewe." Lakini Mungu alimwambia, "Nitakuadhibu kwa sababu ya kuua Habili. Hakuna utakachopanda na ikue. Hautakuwa na rafiki tena, kila mtu atakuchukia."

Halafu Kaini akasema, "Kila mtu atataka kuniua." Mungu aliweka alama kwa Kaini kuzudi watu wote wajue kwamba wakimua Kaini, nao wataadhibiwa zaidi ya Kaini.

Kaini aliwaacha Adamu na Hawa na akaenda kuishi kwa nchi ya Nodi mashariki mwa Bustani ya Edeni. Nodi inamaanisha, 'nchi ya uhamisho.' Baadaye Kaini alioa na akazaawatoto. Alijenga mji. Lakini Kaini na jamii yake hawakumpenda Mungu wala kumtii.

Habili alikuwa amekufa na Kaini alikuwa muuwaji. Adamu na Hawa walitaka mwana atakaye dhibitisha ahadi waliyoahidiwa kwamba atawaondolea adhabu ya dhambi ya kifo. Hawa alipata mwana mwingine. Alimuita Sethi. Na akasema, "Mungu amenipa mwana mwingine badala ya Habili."

Sethi alikua na upendo kwa Mungu. Uzao wa Sethi wote walikuwa haki. Kulikuwa na watu wa aina mbili duniani. Kaini na uzao wake walikuwa waovu. Sethi na uzao wake walikuwa haki.

